**THE SUCCESS PATH EXAMINATION COUNCL (SPEC)**
**Paving the Way to Success**

**102/3** # KISWAHILI

**FASIHI**

**Karatasi ya 3**

**MTIHANI WA PRE-MOCK 2026**
**MACHI 2026**
**Muda: Saa 2½**

---

**Jina**: ………………………………………………………………… **Numbari ya Usajili** ……….

**Shule** ……………………………………………………………. **Mkondo**: ……………………….

**Sahihi ya Mtahiniwa** ……………………………….………… **Tarehe:** ……………………………..

---

**MAAGIZO:**

(a) Andika jina lako na nambari yako ya usajili katika nafasi ulizoachiwa hapo juu

(b) Tia sahihi kisha uandike tarehe

(c) Jibu maswali **manne** pekee

(d) Swali la kwanza ni la lazima

(e) Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Riwaya, Tamthilia,Ushairi na Hadithi Fupi

(f) Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja

(g) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| **Jumla** | **80** | |

## SEHEMU A: USHIAIRI
## SWALI LA LAZIMA

1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.

**LONGA**

Longa Longea afwaji, watabusarika,
Longa uwape noleji, watanusurika,
Longa nenea mabubu, sema na viduko.

Longa usichachawizwe, tamka maneno,
Longa usitatanizwe, mbwa aso meno,
Longa usidakihizwe, kishindo cha funo.

Longa yote si uasi, si tenge si noma,
Longa pasi wasiwasi, ongea kalima,
Longa ukuli kwa kasi, likate mtima,
Longa zungumza basi, liume ja uma.

Longa japo ni kombora, kwa waheshimiwa,
Longa liume wakora, kwani wezi miwa,
Longa bangu na papara, hawakuitiwa,
Longa bunge si kiwara, si medani tawa,
Longa ni simbamarara, wanaturaruwa.

(a) Tambua nafsineni katika nudhumu hii. (alama 1)
(b) Onyesha vile kibali cha utunzi wa mashairi kilivyotumiwa kukidhi mahitaji ya kiarudhi. (alama 3)
(c) Kwa kutoa maelezo mwafaka, tambua bahari **nne** zilizotumiwa na mtunzi kwenye shairi hili. (alama 8)
(d) Onyesha vile shaha alivyofua dafu kutumia mbinu zifuatazo. (alama 5)
(i) Anafora
(ii) Usambamba wa kiusawe.
(i) Usambamba wa kifahiwa/dhamira.
(ii) Tabaini.
(iii)Jazanda
(e) Tambua toni ya shairi hili. (alama 1)
(f) Neno kasi ni adhidadi. (alama 1)
(g) Neno afwaji limetumika kumaanisha nini katika shairi hili. (alama 1)

## SEHEMU B: RIWAYA
**Clara Momanyi: Nguu za Jadi**

**Jibu swali la 2 au la 3**

2. "Pole kaka, huu ndio ulimwengu wetu… ulimwengu unaoendeshwa na sarafu, ndugu. Tumekuwa kama wanyama wa mwitu. N'ambie tofauti i wapi yakhe? Kama wanyama, hatuna tena mipaka ya umri, nasaba au vyeo."
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Fafanua maana ya kitamathali kwenye kauli iliyopigiwa mstari. (alama 2)
   (c) Onyesha jinsi unyama wa msemaji kwenye dondoo ulivyoathiri wengine kwenye jamii. (alama 6)
   (b) Kando na msemaji wa dondoo hili, kuna wahusika wengine walioendeleza utovu wa maadili katika jamii. Thibitisha. (alama 8)

3. Riwaya ya Nguu Za Jadi ni kioo cha nchi za Afrika. Fafanua. (alama 20)

## SEHEMU C: TAMTHILIA
**T. AREGE: *Bembea ya Maisha***

**Jibu swali la 4 au la 5**

4. Si neno mama! (Kimya.) Hakuna kizuri kijacho kwa urahisi. Mazuri hutoka mbali na wakati mwingine yana hadithi za kutisha.

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Bainisha mbinu mbili za kimtindo katika dondoo hili. (alama 4)
(c) Fafanua sifa za msemaji. (alama 6)
(d) Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. (alama 6)

5. (a) Ndiyo ni mgonjwa lakini mume ambaye ni mwanamume kweli hangoji kuelezwa kinafanyika nini."
   (i) Bainisha maudhui yanayojitokeza katika dondoo. (alama 1)
   (ii) Onyesha jinsi maudhui uliyotaja katika (i) yalivyoshughulikiwa katika tamthilia ya *Bembea ya Maisha*. (alama9)

   (b) Ndoa ni bembea. Jadili kwa kurejelea tamthilia ya ***Bembea ya Maisha***. (alama 10)

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

**D.M. Lutomia na P. Muthama (Wah.):** ***Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine***

**Jibu swali la 6 au la 7**

6. **Yussuf Shoka Hamad**: "***Mzimu wa Kipwerere!"***

"Vipi kuhusu usambazaji wa mizigo? Tunahitaji akina mama zaidi maana mzigo ndio kama unavyouona na umejaa humu na hauuzwi kwa wingi! Umelifikiriaje hili?

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Bainisha mbinu **tatu** za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 3)

(c) Eleza sifa **sita** za msemaji katika dondoo hili. (alama 6)

(d) Suala la dawa za kulevya limejitokeza katika hadithi, "***Mzimu wa Kipwerere***." Thibitisha. (alama 7)

7. (a) "Kwa muda wote tuliokaa pamoja, sikufichua siri yoyote ambayo nilijua". Onyesha siri ambazo msemaji hakufichua katika hadithi, "***Kifo cha Suluhu***". (alama 7)

(b) "Ni wajibu wetu wanawake kutetea maisha yetu na yale ya Watoto wetu." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hadithi, "***Nipe Nafasi."*** (alama 13)

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. (a) Maigizo ni nini? (alama 2)

(b) Fafanua sifa zozote **tano** za maigizo. (alama 10)

(c) Eleza dhima ya michezo ya watoto. (alama 8)